# MUUNDO WA MPANGO MKAKATI WA TCRA 2026/27 - 2030/31

## Dira ya Maendeleo Tanzania 2050

Mageuzi ya Kidijitali yenye matarajio ya kuwa na Serikali mtandao inayotoa huduma bora, jumuishi, na zenye ufanisi kwa raia na biashara, kwa lengo lakuimarisha ubora wa huduma za Serikali.

## Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV)

Kukuza matumizi ya TEHAMA

## Sera ya Taifa ya TEHAMA

Kujenga, kusambaza na kutumia TEHAMA, ili kuiwezesha jamii ya kitanzania kuwa na maarifa kupitia matumizi ya TEHAMA.

## Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala 2025 - 2030

Umuhimu wa miundombinu ya mawasiliano katika kujenga, kufanikisha na kudumisha uchumi endelevu, kuinua ubora wa maisha na kuimarisha viwango vya maisha ya Watanzania

## Masuala Muhimu

- Upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa wote
- Kuwezesha na kukuza matumizi ya teknolojia mpya zinazoibukia.
- Unafuu wa gharama za vifaa vya mawasiliano vinavyotumia teknolojia ibukizi.
- Uelimishaji wa umma katika masuala ya kidijitali na uelewa wa watumiaji kuhusu huduma za mawasiliano;
- Kukuza uelewa na ujuzi wa kidijitali katika huduma za mawasiliano;
- Mazingira wezeshi na bora ya kiutendaji katika shughuli za udhibiti wa sekta;
- Kuimarisha usalama wa anga ya mtandao na kukabiliana na udanganyifu mtandaoni
- Uendelezaji wa miundombinu ya kisasa ya mawasiliano.
- Kukuza na kuhamasisha ushiriki katika matumizi ya sayansi na teknolojia ya anga.
- Mageuzi ya kiteknolojia katika huduma za posta na usafirishaji vifurushi na vipeto;
- Uzingatiaji wa sheria, kanuni, miongozo na viwango za huduma za mawasiliano, ubunifu na maudhui ya ndani;
- Usimamizi wa viwango na udhibitisho wa ubora wa vifaa vya mawasiliano;
- Ushirikishwaji wa wadau na katika kusimamia sekta ya mawasiliano.
- Kuimarisha miongozo ya udhibiti ilikwenda sambamba na ukuaji wa teknolojia;
- Utafiti na durusi kuhusu huduma zinazosimamiwa;
- Kuongezeka kwa kasi katika masuala ya ulinzi wa watoto mtandaoni;
- Kuongeza kasi ya mabadiliko ya kidijitali na ufikiaji wa huduma kwa wote;
- Kuhamasisha miundombinu ya mawasiliano inayohifadhi mazingira.
- Kuongeza uelewa wa watumishi kuhusu magonjwa VVU/UKIMWI na yasiyo ya kuambukiza (NCDs) na kuboresha huduma za usaidizi wanaoishi na magonjwa hayo;
- Kuongeza uelewa wa watumishi kuhusu mapambano dhidi ya rushwa
- Kuongeza ufanisi wa taasisi katika kusimamia rasimali za mawasiliano.

## Dira

Jamii iliyowezeshwa na huduma jumuishi na endelevu za mawasiliano.

## Dhima

Kusimamia huduma za mawasiliano kwa ustawi wa Jamii ya Watanzania.

## Tunu Kuu

- Weledi
- Ubunifu
- Ushirikiano
- Wepesi wa Kujirekebisha

## Lengo la Maendeleo

- Kuboresha huduma za Mawasiliano salama, za ubunifu na jumuishi.

## Malengo ya Kimkakati

- Kukuza miundombinu na matumizi ya mawasiliano yenye uimara, usalama na uwezo wa kustahimili changamoto."
- Kuongeza upatikanaji na ubora wa huduma za mawasiliano kwa gharama nafuu
- Kuimarisha uwezo wa taasisi.
- Kuimarisha utendaji na ufanisi wa huduma zinazosimamiwa na ushirikishwaji wa wadau; na
- Kukuza uvumbuzi kwenye huduma za mawasiliano Sambamba na uzalishaji na uhifadhi wa maudhui ya ndani.

## Matokeo ya Mkakati

- Kupatikana kwa huduma za mawasiliano zilizo za uhakika na salama;
- Kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za mawasiliano zilizo bora na nafuu ;
- Jamii yenye kuzalisha na kutumia maudhui ya ndani;
- Kuboresha uzingatiaji wa kanuni na utendaji wa soko la mawasiliano.
- Kuongezeka kwa ufanisi wa kiutendaji wa taasisi.
- Kuongeza uelewa wa umma kuhusu huduma za mawasiliano;
- Kuongeza ufikiaji na matumizi ya intaneti ya kasi.